

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA

Anuani ya simu: "UCHUNGUZI"  
Simu nambari: +255 28 2982501

Nukushi nambari +255 28 2982501  
Email: rbcgeita@pccb.go.tz



MKUU WA TAKUKURU (M),  
MTAA WA NYANZA  
S.L.P 38,  
Geita

21/12/2020

**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI.**

**MENEJA MZANI BWANGA AHUKUMIWA KIFUNGO KWA MAKOSA YA RUSHWA.**

Mahakama ya Wilaya ya Chato mkoani Geita imemhukumu aliyekuwa Meneja wa mzani wa kituo cha Bwanga kilichopo wilaya ya Chato **Bw. DAUDI JAMES KADIKILO** kwa makosa ya Rushwa kinyume na kifungu cha 15(1)(a) na (2) cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na. 11/2007 katika kesi ya Jinai Na. **100/2019** iliyokuwa inaendelea mahakamani hapo.

Akisoma hukumu hiyo tarehe 18/12/2020, Mheshimiwa Hakimu wa Mahakama ya wilaya ya Chato, **Mhe. Erick Kagimbo** alisema mahakama imemkuta na hatia Mshitakiwa katika makosa yote manne kama alivyoshitakiwa, kwamba:

- **Kwa kosa la kwanza** Mshitakiwa alitakiwa kulipa faini ya **shilingi 900,000/=** au kwenda jela miaka mitatu,
- **Kosa la pili** Mshitakiwa alitakiwa kulipa faini ya **shilingi 800,000/=** au kifungo cha miaka mitatu (3) jela **na**
- **Kosa la tatu** Mshitakiwa alitakiwa kulipa faini ya **shilingi 1,000,000/=** na kifungo cha miaka mitatu jela kwa pamoja
- **Kosa la nne** Mshitakiwa akitakiwa kulipa faini **shilingi 8000,000/=** na kutumikia kifungo cha miaka mitatu jela.

Pamoja na adhabu hiyo Mahakama ilitoa amri ya kutaifishwa kwa gari la Mshitakiwa aina ya **Suzuki Escudo** iliyotumika kubeba fedha za rushwa yenye namba ya Usajili **T176DMP** pamoja na simu aina **Tecno** iliyotumika kufanya miamala ya fedha za rushwa kupitia njia ya MPesa.

Mhe. **Erick Kagimbo** alifafanua kwamba ushahidi uliowasilishwa na upande wa Jamhuri umethibitisha pasi na shaka kwamba mnamo tarehe 12/03/2019 Mshitakiwa aliomba Rushwa ya **shilingi 1,000,000/=** kutoka kwa **Phabian Peter Shigadu** ili asimchukulie hatua baada ya kukamatwa kwa kosa la kukwepa mzani wa TANROADS wa Bwanga akiwa amepakia mchanga wa kuchenjulia dhahabu, na kwamba mnamo tarehe 12/3/2019 Mshitakiwa alipokea sehemu ya fedha alizomba kiasi cha **shilingi 100,000/=** kutoka kwa dereva wa gari hiyo, na tarehe 13/3/2019 Mshitakiwa alipokea **shs. 100,000/=** kwa njia ya mpesa na kiasi cha **shilingi 100,000/=** alizipokea kwenye mtego wa Rushwa na hivyo kufanya jumla ya fedha alizopokea kuwa **shilingi 300,000/=**.

Kesi hii ilikuwa ikiendeshwa na Mwendesha Mashitaka wa TAKUKURU mkoa wa Geita Ndg. **KELVIN MURUSURI**.

Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Geita **Bw. Leonidas R. Felix** anatoa wito kwa watumishi wa Umma Mkoani Geita kuzingatia viapo na maadili ya kazi zao aidha amewataka wananchi wa Mkoa wa Geita kuendelea kutoa taarifa za vitendo vya Rushwa ili Watuhumiwa wachukuliwe hatua za kisheria ili kukata mnyororo wa Rushwa.

Imetolewa na:

Bw. Leonidas R. Felix.

Mkuu wa **TAKUKURU (M) GEITA**